

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
(Jeshi la Magereza)

Anwani ya Simu: "MAGEREZA"
Simu namba: (+255) 026 2323300
Fax: (+255)-026:2323260
Email: cgp @prisons.go.tz



OFISI YA KAMISHNA JENERALI WA MAGEREZA
MAKAO MAKUU YA MAGEREZA
ENEO LA MSALATO,
BARABARA YA ARUSHA,
S.L.P. 1176,
DODOMA.

30 Mei, 2022

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA AJIRA ZA
JESHI LA MAGEREZA KWA MWAKA 2022**

1. Serikali imetoa Kibali cha Ajira za Jeshi la Magereza. Hivyo, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, anatangaza nafasi za ajira mbadala 1,241 za kujiunga na Jeshi kwa Mwaka 2022. Jeshi litaajiri kwa kuzingatia vigezo vinavyohitajika kulingana na maelekezo ya Serikali. Hivyo Waombaji wote wanaotaka kujiunga na Jeshi la magereza wanatakiwa wawe na sifa zilizoanishwa hapa chini: -

a. **Elimu Ya Kidato Cha Nne (Wasio Na Ujuzi)**

- (1) Awe ni raia wa Tanzania
- (2) Awe amemaliza kidato cha Nne na kupata ufaulu wa daraja la1-IV
- (3) Awe na umri kati ya miaka 18-25
- (4) Awe kwenye mafunzo katika Kambi za JKT au awe amefuzu tayari mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
- (5) Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini
- (6) Asiwe ameo/kuolewa na Awe na siha njema
- (7) Awe hajawahi kupatikana na hatia katika Makosa ya Jinai
- (8) Urefu usiopungua futi 5'4" (wanawake) na futi 5'7" (wanaume)

b. **Elimu Ya Kidato Cha Nne (Wenye Ujuzi)**

- (1) Awe ni raia wa Tanzania
- (2) Elimu ya Kidato cha Nne (Wenye ujuzi)

- (3) Awe amehitimu Astashahada katika fani ya udereva wa Trekta toka Chuo chenye usajili wa VETA na leseni ya udereva daraja G”
- (4) Awe na umri kati ya miaka 18-33
- (5) Awe na siha njema
- (6) Awe kwenye mafunzo au awe amefuzu tayari mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
- (7) Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini
- (8) Asiwe ameo/kuolewa
- (9) Awe hajawahi kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai
- (10) Urefu usiopungua futi 5’4” kwa wanawake na futi 5’7” kwa wanaume

Utumaji Barua za Maombi

2. Barua za maombi lazima ziambatanishwe na nakala zifuatazo:-
 - a. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa (Birth Certificate)
 - b. Nakala ya Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Kidato cha Nne (Academic Certificate)
 - c. Nakala ya Cheti cha Kumaliza Shule (School Leaving Certificate)
 - d. Cheti cha Uthibitisho wa siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali
 - e. Nakala ya Kitambulisho au Namba ya Utaifa (NIDA)
 - f. Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au barua ya uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kikosi
 - g. Picha mbili (2) za Passport Size
 - h. Nakala ya cheti cha ujuzi husika kinachotambulika na Mamlaka za Elimu nchini (kwa wale wenye ujuzi)
 - j. Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa
 - k. Wasifu (Curriculum Vitae - CV) kwa wale wenye ujuzi tu
 - l. Matokeo ya muda (Testimonials, “Provisional Results”, Statement of Results” na hati za matokeo ya Kidato cha Nne (Form IV Notification Examination Results) HAVITA KUBALIWA isipokuwa kwa wahitimu wa Mwaka 2021 tu.

Utaratibu Wa Kutuma Maombi


3. Taratibu za utumaji wa Barua za Maombi ni kama ifuatavyo:-
- a. Kwa waombaji wa elimu ya kidato cha Nne (wasio na ujuzi) maombi yao yatumwe kwa Mkuu wa Gereza wa Wilaya husika na kwa Wilaya zote ambazo hazina Gereza maombi yao yatumwe kwa Mkuu wa Gereza lililo jirani. Maombi haya yatatakiwa kujadiliwa katika Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na baadae Kamati za Ulinzi na Usalama ya Mkoa husika
 - b. Kwa waombaji wa Kidato cha Nne (wenye ujuzi) maombi yatumwe kwa:-
Kamishna Jenerali wa Magereza,
Barabara ya Arusha,
Eneo la Msalato,
P.O.Box 1176,
DODOMA.

Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta. Barua zitakazowasilishwa kwa njia ya mkono au barua pepe (email), hazitapokelewa na kufanyiwa kazi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 Juni, 2022.**

NB: Waombaji waliofukuzwa katika kozi za kijeshi za mafunzo ya awali hawaruhusiwi kuomba tena

Inakumbushwa kuwa ni kosa la jinai kuwasilisha nyaraka za uongo (Forged Documents). Kwa yeyote atakayebainika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye Vyombo vya Sheria. Inasisitizwa kwamba maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa na:



Maj Gen SM Mzee, ndc

KAMISHNA JENERALI WA MAGEREZA

Nakala

Wakuu wa Mkoa yote

Wakuu wa Wilaya zote